TANGAZO LA SERIKALI NA. 882 la tarehe 1/12/2023

SHERIA YA UMEME,
(SURA YA 131)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 22(1) na 45)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA SHUGHULI ZA UZALISHAJI, UPELEKAJI NA USAMBAZAJI WA UMEME, 2023

Jina

TS. Na. 452 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji wa Umeme za Mwaka 2023, na zitasomwa pamoja na Kanuni za Shughuli za Uzalishaji, Upelekaji na Usambazaji wa Umeme ambazo zitarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kifungu wezeshi

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika vifungu wezeshi kwa kufuta tarakimu "14(5)".

Marekebisho ya jumla

3. Kanuni kuu zinafanyiwa marekebisho ya jumla-
(a) kwa kufuta maneno "Bila kujali" popote yalipotumika, isipokuwa katika kanuni ya 75(2), na badala yake kuweka maneno "Bila kuathiri";
(b) kwa kufuta maneno "mwenye leseni" popote yalipotumika na badala yake kuweka maneno "mmiliki wa leseni".

Marekebisho ya kanuni ya 2

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 2 kwa kuongeza aya "c" kama ifuatavyo :

"(c) usimamizi wa chumba cha udhibiti.".

Marekebisho ya kanuni ya 3

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuweka tafsiri za misamiati katika mtiririko wa kialfabeti.

Marekebisho ya kanuni ya 5

6. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 5(2)-

(a) katika aya (b) kwa kubadili mpangilio wa aya ndogo za "a." na "(vi)" kuwa aya ndogo za "(vi)" na "(vii)" mtawalia; na

(b) katika aya (c)-

(i) kwa kubadili mpangilio wa aya ndogo ya (i) iliyopo baada ya aya ndogo ya (ix) kuwa aya (d);

(ii) kwa kubadili mpangilio wa aya ndogo zinazofuata za (ii) hadi (v) kuwa aya ndogo za (i) hadi (iv) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 14

7. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 14 kwa kuongeza maneno "ndani ya siku kumi na nne" baada ya neno "mwombaji".

Marekebisho ya kanuni ya 17

8. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 17(3) kwa kufuta neno "msuluhishi" lililopo katika aya (b) na badala yake kuweka neno "msimamizi".

Marekebisho ya kichwa cha Sehemu ya Nne

9. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kichwa cha Sehemu ya Nne kwa kufuta neno "MASHAETI" na badala yake kuweka neno "MASHARTI".

Marekebisho ya kanuni ya 35

10. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 35-

(a) kwa kufuta maneno "ndani ya saa ishirini na nne" yaliyopo katika maneno ya utangulizi;

na

(b) kwa kuweka maneno "ndani ya saa ishirini na nne" kabla ya neno "kuwafahamisha" lililopo mwanzoni mwa aya (b).

Marekebisho ya kanuni ya 48

11. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 48 kwa kufuta na kuandika upya kanuni ndogo za (1) na (2) kama ifuatavyo:

"(1) Mmiliki wa leseni ya upelekaji umeme anapaswa, baada ya maombi ya mwendeshaji wa mfumo na soko la umeme, kutoa taarifa zote kuhusu miundombinu ya upelekaji umeme.

(2) Taarifa inayoelezewa katika kanuni ndogo ya (1) inaweza kuwa nyongeza kwa taarifa ambayo inatakiwa kutolewa chini ya kanuni za soko au chini ya leseni.".

Dodoma,
……………….…….., 2023

JAMES A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*